**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TANGAZO LA MWALIKO WA WAANGALIZI WA NDANI WA UCHAGUZI KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA PERAMIHO HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA, MKOA WA RUVUMA NA UDIWANI KATIKA KATA YA SHIWINGA ILIYOPO JIMBO LA MBOZI, HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI, MKOA WA SONGWE

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Peramiho lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Songea Mkoa wa Ruvuma na Udiwani katika Kata ya Shiwinga iliyopo Jimbo la Mbozi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Alhamisi tarehe 26 Februari, 2026 katika jimbo na kata tajwa.

Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 13(1) na (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatoa mwaliko kwa waangalizi wa uchaguzi wa ndani wenye nia ya kuangalia uchaguzi.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi za ndani zenye nia ya kuangalia uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Peramiho na Udiwani katika Kata ya Shiwinga.

Taasisi na asasi zenye nia ya kuangalia uchaguzi huo ziwasilishe maombi kwa kutumia kiunganishi (*link*) kifuatacho *https://ams.inec.go.tz*

Barua ya maombi pamoja na mambo mengine itatakiwa kuainisha mambo yafuatayo: -

i. Anuani kamili ya taasisi au asasi husika;

ii. Mahali ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi (*Physical address*);

iii. Shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;

iv. Sehemu ambazo taasisi au asasi inapenda kwenda kuangalia uchaguzi;

v. Idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na majina na taarifa zao binafsi;

vi. Majina na namba za simu za viongozi watatu wa taasisi au asasi husika;

vii. Ikiwa taasisi au asasi ya ndani inahusisha viongozi ambao si raia wa Tanzania, viongozi wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa ni lazima wawe Watanzania;

viii. Nakala au kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi husika; na

ix. Nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika.

Maombi hayo yatapokelewa kuanzia **tarehe 20 Januari, 2026 hadi 26 Januari, 2026.**

**Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la uangalizi wa uchaguzi kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.**

**Aidha, maombi yatakayotumwa kwa njia tofauti na mfumo ulioainishwa katika tangazo hili hayatafanyiwa kazi.**

Imetolewa leo tarehe **19 Januari, 2026** na:

Kailima, R. K
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**